LAWYERS' ENVIRONMENTAL ACTION TEAM (LEAT)

Research, Advocacy and Training on Environmental / Natural Resource Law and Policy and the Promotion of Human Rights
Website: http://www.leat.or.tz

Tel: +255 22 2780859
Fax: +255 22 2781098
Email: info@leat.or.tz
Website: http//www.leat.or.tz

Mazingira House, Plot No. 428
Mazingira Street, Mikocheni B
P.O.Box 12605
Dar es Salaam

29 Aprili 2022

TAARIFA KWA VYOMBO VVA HABARI

UCHAFUZI WA MAZINGIRA UMEKITHIRI NCHINI NA VYOMBO HUSIKA VIMESHINDWA KUPAMBANA NAO

Ndugu Waandishi wa Habari.

Katika siku za hivi karibuni kumekuwa na matukio ya kushangaza na kusitikisha sana ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira unaofanywa nchini hasa katika Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Mara. Moja mnamo tarehe 5 hadi 6 Aprili 2022 kulikuwa na umwagikaji wa mafuta katika eneo la Forodhani (Ferry) na kutapakaa baharini na hivyo kuleta uharibifu mkubwa si wa mazingira tu bali pia viumbe wa baharini na vyanzo vya mapato kwa wavuvi na wale wanaotegemea sekta ya uvuvi. Mnamo tarehe 6 Aprili 2022 Mkuu wa Wilaya ya llala, Nd. Ng'wilabuzu Ludigija alitembelea eneo hilo na kuthibitisha pasi na shaka kuwepo kwa uchafuzi huo wa mazingira na kunukuliwa na vyombo vya habari https://www.youtube.com/watch?v=GIY31YTS 7Q akitoa tahadhari kwa wakazi wa Dar es Salaam kutonunua mafuta yaliyochotwa na watu ambao waliyachota na kuyatoa baharini. Hata hivyo alitoa tuhuma ya jumla kuwa mafuta hayo yalimwagwa baharini na meli isiyojulikana!.

Kauli hiyo inashangaza na haingii akilini kwani eneo zima la Feri pale Kivukoni lipo chini ya Mamlaka ya Bandari ya Tanzania na ina mamlaka ya kudhibiti uchafuzi wowote ule wa mazingira ufanywao na meli. Kwamba "meli" hiyo hakuweza kubainika ni uthibitisho kuwa Mamlaka ya Bandari ya Tanzania imeshindwa kutekeleza wajibu wake kama ambavyo imepewa na Sheria ya Bandari (Ports Act No 17 of 2004). leleweke kuwa hakuna meli yoyote

ile inayoweza kuingia katika maji ya ndani ya nchi yetu bila kibali cha nchi yetu na kuwa meli yoyote ile iingiayo katika maeneo ya maji ya nchi yetu inalazimishwa na sheria zetu na sheria za kimataifa kuheshimu sheria za nchi yetu. Na kwa kuwa meli zinazotia nanga katika bandari zetu zinakuwa na kibali basi ni kuwa "meli" hiyo ilipata kibali hicho na kama kweli ndiyo iliyomwaga mafuta hayo katika eneo hilo basi umwagaji huo uliruhusiwa au kufumbiwa macho na viongozi wa Mamlaka ya Bandari ya Tanzania. Aidha, uchafuzi huo pia umefumbiwa macho na Baraza la Taifa la Utunzaji Mazingira (National Environment Management Council (NEMC) ambalo lina mamlaka ya kuhakikisha kuwa uchafuzi wowote ule wa mazingira nchini unapingwa vita na wachafuzi wanachukuliwa hatua stahiki.

Kana kwamba hiyo haitoshi usiku wa tarehe 6 kuamkia tarehe 7 Aprili 2022 moto mkubwa ulizuka katika eneo la kuhifadhia mafuta machafu eneo la Kigamboni. Eneo hilo lipo chini ya Mamlaka ya Mafuta ya TAZAMA. Moto huo ulisababisha taharuki kubwa kwa wakazi wa Kigamboni na kuchafua hewa kwani anga ilijaa moshi mzito wenye sumu. Hakuna hatua za maana zilizochukuliwa kubaini chanzo cha moto huo na kuwawajibisha waliousababisha au kuzembea na kusababisha. LEAT ilitembelea eneo hilo mnamo tarehe 7 Aprili 2022 na kubaini kuwa eneo hilo ni la hatari na li karibu na Jalala la Wazi la kutupa taka na kuwa pindi moto ukizuka katika Jalala hilo kutokana na kuvuja kwa hewa ya methane basi mafuta yaliyopo pale nayo yatapata moto na kulipuka. La kushangaza ni hatua ya kuweka askari wa kampuni binafsi na polisi kuzingira eneo hilo wakiwa hawana hata vifaa vya kujikinga na hewa chafu na kali katika eneo hilo.

Kama kwamba wachafuzi walikuwa wamekubaliana kuwa watekeleze uchafuzi wao, mnamo tarehe 6 Aprili wananchi wa Temeke Sandali walijitokeza hadharani na kuzuia magari yanayopita katika maeneo yao yakiwa yamebeba kemikali za Sulfur ambazo zimehifadhiwa katika maghala ya wazi ya Kampuni ya Lake Group iliyoko eneo hilo. Hadi hivi sasa Serikali haijachukua hatua ya kusitisha uchafuzi huo mkubwa.

Sambamba na hilo mnamo mwezi Machi na Aprili mwaka huu tumeshuhudia vitendo vya uchafuzi wa mazingira katika eneo la Mto Mara na kuundwa kwa Timu ya Uchunguzi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Raisi, Dakta Selemani Jaffo, ikiongozwa na Prof. Samwel Manyele ambayo badala ya kuleta majibu juu ya chanzo cha uchafuzi ilizidisha mkanganyiko kwa kutoa taarifa mbili zinazokinzana. Tunashukuru kuwa hata Bunge letu

lilibaini upotovu wa Ripoti hiyo na kuikataa. Hata hivyo tulisikitishwa sana na kauli za Waziri Jaffo kuwa wakati Wabunge wanajadili Ripoti hiyo waangalie masilahi mapana ya nchi ikiwa ni pamoja kuvutia wawekezaji.

Tunapenda kusema kuwa hakuna uwekezaji wowote ule ambao una thamani zaidi kushinda maisha ya Watanzania na mazingira yao. Mchafuzi yeyote yule anapochafua mazingira lazima achukuliwe hatua stahiki. Na pale uchafuzi unapofanywa ni lazima kiwango cha uchafuzi kibainike na kutajwa kwa uwazi kabisa. Kwa kuwa uchafuzi wa mito na Maziwa kunahatarisha viumbe maji wote na watumiaji wa maji ni lazima pindi uchafuzi unapotokea taarifa ya haraka na ya wakati itolewe kwa umma na kutoa tahadhari na miongozo ya vitu gani vifanywe na Serikali ichukue hatua za kusafisha mazingira yaliyoaharibiwa na kudai kurudishiwa gharama ilizotumia kutoka kwa mchafuzi. Kuficha kutoa taarifa kwa kisingizio cha kulinda masilahi mapana ni kushiriki katika kukiuka Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania inayotoa hakikisho la haki ya kuishi na hifadhi ya haki hiyo kutoka kwajamii. Hatutaki kuamini kuwa Waziri Jaffo halijui hilo.

Aidha, wiki iliyopita kuliripotiwa uchafuzi wa Mto Tigite katika eneo la Nyamonyo wilaya ya Tarime mkoani Mara kutokana na kutoboka kwa bwawa la kuhifadhia maji machafu kutoka Mgodi wa North Mara. Mara baada ya uchafuzi huo mwananchi mzalendo na mzaliwa wa eneo hilo Mzee Nyaronyo Kicheere alijitokeza wazi katika Kipande cha video mtandaoni na kushangaaa kutoona maji hayo machafu katika mabwawa hayo. Kesho yake tarehe 22 Aprili 2022 Waziri wa Madini Dakta Dotto Biteko alitembelea eneo hilo akiwa ameambatana na Mkurugenzi Mtendaji wa NEMC, Dakta Mhandisi Samweli Mafwenga iliitoza North Mara shilingi bilioni moja. Hiyo ni faini ndogo sana kwani mwaka 2019 kampuni hiyo ilitozwa faini ya dola 2.4 milioni kwa uchafuzi kama huo. Kutokana na kampuni hiyo kuwa mchafuzi sugu ilitegemewa kuwa faini ya juu kabisa ndiyo ambayo ingetozwa.

Wakati hayo yanatukia wiki hii tumeshuhudia ukataji wa miti iliyo pembezoni mwa Barabara ya Ali Hassani Mwinyi katika maeneo ya Daraja la Salender Jijini Dar es Salaam. Ukataji wa miti hiyo ilipandwa na kutunzwa kwa gharama kubwa katika eneo hilo ili kupambana na mmomnyoko wa udongo kutokana na mawimbi ya bahari na kutoa kivuli kwa watembea kwa miguu umefanywa kwa kibali cha Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni bila kufuata kanuni za utunzaji mazingira. Ajabu yake viongozi wa Manispaa hiyo wanadai kuwa miti

hiyo ilikuwa inaharibu barabara na nyumba zilizo jirani. Wakati wakidai hivyo wametoa ruhusa kwa Kampuni Moja ya Minara ya Mabango Makubwa ya Barabarani kujenga Mnara wa Bango kubwa ili kuendesha biashara ya matangazo kwa njia ya bango. Ni wazi kuwa ukataji huo umefanywa kwa lengo la kuwezesha kampuni hiyo kufanya biashara ya matangazo kwa njia ya mabango. LEAT inalaani hatua hiyo ya Manispaa ya Kinondoni. Aidha, inashangazwa na kitendo cha TANROADS ambayo ndiyo mamlaka husika ya eneo hilo kutochukua hatua za kuzuia ukatwaji wa miti hiyo na kutosimikwa kwa bango hilo kubwa.

Ni kwa misingi hiyo LEAT inataka mambo yafuatayo:

1. Kuchukukuliwa kwa hatua za kisheria za kuwashika na kuwafikisha mahakamani wote waliohusika na umwagaji wa mafuta katika eneo la Feri Jijiji Dar es Salaam;

2. Kuwawajibisha viongozi wa Mamlaka ya Bandari ya Tanzania kwa kutosimamia kikamilifu utekelezwaji wa Sheria ya Bandari Namba 17 ya 2004,

3. Kufungwa mara moja kwa bwawa la mafuta machafu eneo la Kigamboni pamoja na Jalala la Wazi lililo jirani na bwawa hilo;

4. TAZAMA iendeshe shughuli za usafishaji mafuta kwa kufuata Sheria ya Utunzaji Mazingira nchini na kutomwaga mafuta machafu katika eneo hilo tena;

5. Uchunguzi juu ya uharibifu wa mazingira ya Mto Mara ufanywe na vyombo huru vikiongozwa na wataalamu wanaoaminika wa ndani na nje na mchafuzi akibainika achukuliwe hatua kali sana za kisheria;

6. Kufanywa kwa uchunguzi wa kina wa athari za uchafuzi wa Mto Tigite, Mara na Ziwa Victoria kutokana na uchafuzi uliofanywa na Kampuni na North Mara wiki iliyopita na kutoa fidia ya haki na inayostahili kwa waathirika wote wa uchafuzi huo;

7. Kusitishwa mara moja ukatwaji wa miti katika eneo la Daraja la Salender na kuwawajibisha maofisa wa Manispaa ya Kinondoni na TANROADS waliotoa kibali cha kukatwa miti katika eneo hilo;

8. Kampuni iliyokata miti katika eneo la Salender iamuriwe kuipanda na kuitunza miti mingine katika eneo hilo hadi itakapofikia ukubwa wa miti iliyokatwa na kuzuiwa

kufanya biashara ya mabango katika eneo hilo na kuondoa mabango yake katika eneo hilo;

9. Utunzwaji wa mazingira ni lazima utiliwe mkazo na uchukuliwe kama nguzo muhimu ya ulinzi wa uhai wa maisha ya Watanzania. Kupuuzia utunzwaji wa mazingira ndiko kunakosababisha mabadiliko ya tabia nchi, magonjwa ya mlipuko, magonjwa ya mfumo wa maisha ikiwa ni pamoja na magonjwa ya kansa na shinikizo la damu;

10. Nchi isiyotunza mazingira yake ni nchi isiyoendelea na haiko katika safari ya kuendelea bali safari ya kuangamia. Shughuli za watu zisizoheshimu utunzaji wa mazingira ni shughuli haramu na hazina manufaa kwa taifa letu kwani mwisho wa siku zitaligharimu taifa kwa kulazimika kutibu madhara ya uharibifu huo;

11. NEMC itekeleze majukumu yake na iache kufuata matamko ya wanasiasa wanaotoa miongozo inayoegemea malengo binafsi ya wanasiasa badala ya mazingira na ustawi mzuri wa nchi yetu; na

12. LEAT kwa upande wake itafungua kesi za masilahi ya umma dhidi ya mamlaka na vyombo vilivyofumbia macho uchafuzi na uharibifu huu wa wazi wa mazingira.

Imetolewa Jijini Dar es Salaam leo tarehe 29 Aprili 2022.

Dkt. Rugemeleza A.K. Nshala
Mkurugcnzi Mtendaji